# Tutakuwa na furaha kama... tutajua kuunda mkondo wetu

Heri wenye moyo safi, maana watamwona Mungu (Mt. 5,8)

## Lengo

- Jifunze kutambua mambo yanayoweza kuhatarisha usafi wa moyo
- Imarisha bidii ya kufanya maamuzi kulingana na maadili yako wenyewe

## Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mang'amuzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"



## Shughuli ya utambulisho

**AINA:** igizo

**Muda:** kama dakika 30 hivi

**VIFAA:** tiketi zenye majukumu mbali mbali katika historia

**UENDESHAJI:** Kila mvulana au msichana anapewa tiketi iliyoandikwa jukumu lake. Wanahitajika wahusika maalumu watatu, wengine wote wanawakilisha kundi. Vijana wengine hawatakiwi kujua majukumu ya rafiki zao lakini muhamasishaji ni lazima ajue.

- Mtazamaji: hukubaliani na kile ambacho darasa linafanya, lakini baada ya kujaribu kusema chochote utakubaliana na wanachofanya wengine kwa hofu ya kutengwa.
- Mwenye fujo: hukubaliani na kile ambacho darasa linafaya na unaona kuwa ni vigumu kubadili wazo lao. Unakasirika na kujibu kwa kutumia maneno mazito.
- Thabiti na jasiri: hukubaliani na kile ambacho darasa linafanya. Hata kama ni vigumu, utabaki thabiti katika maadili yako na utatafuta mbinu ya kuwashirikisha wengine wazo lako.
- Sehemu ya kundi: linakubaliana kabisa na darasa zima.

Baada ya kugawa majukumu vijana wanapendekezwa kuanza historia ifuatayo: *"kwa wiki moja nilienda Uswisi pamoja na darasa langu lote kimasomo. Mwalimu aliyetusindikiza alitupatia uhuru mkubwa. Jioni ya kwanza tulienda katika kijiji kimoja na rafiki zangu wakaanza kunywa pombe na kuvuta sigara. Sikuupenda mwenendo wao, hasa matumizi yao bila kipimo ..."*
Kundi liigize mara tatu jinsi mwisho wa historia utakavyokuwa, kwa kuwafanya wale wahusika watatu ( mtazamaji, mwenye fujo na yule thabiti na jasiri) waingilie kati.

**HITIMISHO:** Fungua nafasi kubwa ya mazungumzo kati ya wote.

- Wale wahusika watatu wameenenda kwa namna tofauti. Je, hii inaweza kubadili majibu ya kundi?
- Ni lipi kati ya maigizo matatu, hutokea mara kwa mara kati ya vijana wenzenu?
- Ni katika hali gani ilikuwa vigumu kwenu kuwa waaminifu kwa maadili yenu, kwa kile mnachokiamani? mlijibuje?

Halafu pendekeza kwa vijana wasome mang'amuzi "Nilijua kuwa siko peke yangu" kugundua kama O. Alishiriki kweli katika hali hii.

## Tuishi hivi

### Nilijua kuwa siko peke yangu

Nilisafiri kwenda Uswisi kwa wiki moja pamoja na darasa langu lote. Mwalimu aliyetusindikiza alitupatia uhuru mkubwa. Jioni ya kwanza tulienda mahali fulani na wanafunzi wenzangu wakaanza kunywa pombe na kuvuta sigara. Sikuupenda mwnenendo wao, hasa kule kutumia bila kipimo. Niliamua kwenda zangu na kutoshiriki tena katika matembezi yao. Hata kama wangenidhihaki, nilijuwa kuwa siko peke yangu: gen 3 wote duniani wanaishi kinyume cha mkondo. Nilipotoka pale mahali, mwenzangu mmoja aliungana nami: pamoja tulifanya matembezi mazuri sana ya kuungalia mji usiku. Jioni ya pili tulijaribu kujadiliana kwa undani pamoja na wenzetu lakini bila mafanikio. Jioni ya tatu tuliandaa ratiba ambayo hata rafiki zetu waliishiriki hata kama hawakuwa tayari, lakini waliiheshimu.

*(O. - Germania)*

## Ujumbe mzuri

Katika darasa langu kuna jopo kwa ajili ya kubadilishana mawazo na habari. Kwa kawaida hutumiwa na wavulana tu kwa ajili ya vitu vya kuuza na pia kuweka picha mbaya. Nilitaka kuishi kinyume cha mkondo, siyo kwa kuwapinga bali kuweka kitu tofauti cha ujumbe mzuri na wenye kujenga.

Nilichukua karatasi kubwa la rangi lenye katuni za Gibì na DoppiaW na chini yake niliweka sahihi yangu. Rafiki zangu walifurahia wakaniomba niwe napeleka katuni moja kila wiki. Hata mwalimu mmoja alitaka kujua zaidi. Nilipomwambia kuwa zile katuni nilikuwa nazichukua kutoka kwenye jarida la 'New City', aliamua kujisajili.

Sasa hata rafiki yangu ameanza kubandika ujumbe mzuri kwenye ubao wa matangazo.

*M. – Brasilien*

Kwangu ilitokea...

Kwa undani

Chiara, kwa kuniona nikiishi 'kinyume cha mkondo', rafiki zangu wanatakiwa kuguswa na kuniuliza kwa nini... lakini si hiyo. Wao wanajua fikra zangu na uchaguzi wangu wa maisha. Wananiheshimu, hawanisumbui, lakini wanabaki kuwa watu wasiojali, kama vile haiwahusu. Kwa nini iko hivi? Unaweza kunipa ushauri gani

*Chiara Lubich, Buenos Aires, 12 Aprili 1998 – Majibu kwa wanafocolare wa Argentina*

## MASHAMBULIZI YA UPENDO

Sasa wewe unasema unaenda kinyume cha mkondo: Vizuri! Lakini haitoshi. Kwenda kinyume cha mkondo maana yake ni kuthamini ubikira, maana yake ni kuthamini utulivu, maana yake ni kuthamini..., vitu hivi vyote. Haitoshi. Hata wewe inakubidi upambane na wengine.

Sisi duniani, tuwe katika mapambano, kwa kuwapenda wengine, au tutaangamizwa, tutapoteza, tutashindwa. Sisi hatuwezi kubaki duniani hivi, bila kufanya chochote, kwa kwenda kinyume cha mkondo kidogi tu. Hakika hawatakuangalia.

Lakini wewe ukianza kuwafinya, kuwapenda, kuwatumikia, kufanya kitu fulani..., kuwafinya kwa maana nzuri ya neno, kutoa huduma, kufanya kitu fulani, watafungua macho, watasema: «Ni nani anakufanya ufanye hivi?». Halafu polepole yatakuja maelezo... na wewe usiache kamwe kupenda, wewe endelea kupenda: yeye anahitaji peni, mwazime; anahitaji kuandika maelezo, mwazime; anahitaji kitu kingine... kama uko shuleni n.k.



Cha muhimu hapa si sana kutetea mkondo wetu, bali ni kuudhi ulimwengu kwa upendo, hivyo tutaushinda.

# TOA MFANO KWA MATENDO

Leo vijana wanagundua tena kwenda kinyume cha mkondo. Lakini pia kuna hatari ya kukana kwa nje tu yale yote yanayowazunguka.
Tufanyeje kuwaelewesha ile namna ya kweli ya kwenda kinyume cha mkondo?

Be', unanipa habari njema, sikuwa najua hili kwamba vijana wanagundua tena wazo la kwenda kinyume cha mkondo.

Unajua kuwa vijana ni wa ajabu! Wana kitu kipya daima, daima wanafaulu kuvutia kwa sababu ya hayo mabadiliko yao, nayo yanawafanya wabadilike katika mazuri.

Mimi ningesema, kwanza kabisa, wewe inabidi utoe mfano, na uwafanye waelewe kwamba wewe unaenda kinyume cha mkondo zaidi yao, kwa sababu wewe unamfuata Yesu ambaye mara nyingi ni ishara ya utata, haswa katika utata wa dunia. Na wewe inabidi uwe mfano katika vipengele vingi.



*Chiara Lubich, Napoli, 3 Mei 1996, kwa jumuiya ya Napoli*

Kwa mfano: wewe unaishi upeo, unatumia utamaduni wa kutoa, mbele ya wote wanaotaka kupata.

Wewe unajionesha safi, wewe ni gen safi, na unajua kuwa wengine wana maraha, ya mambo yote mabaya. Wewe una msamaha: kwa mfano, mtu akikuudhi wewe unamsamehe, wakati wengine wanalipiza kisasi.

Hivyo hata wewe, unawapenda wazazi wako wakati kwa kawaida huwa kuna utata kati ya vizazi. Wewe unapenda vitu ambavyo wengine labda wanavitupilia mbali.

Wewe unapenda hata uchungu; wengine wanakufurahia kwa sababu wao badala yake wanautupilia mbali uchungu. Mpaka unafikia kukabiliana na kifo hata kwa utulivu fulani, kwa sababu unajua kuwa Paradiso itakuwa nzuri zaidi ya hapa.

Wewe unawapenda wote, hata wale wa jamii nyingine, wakati sasa kuna ubaguzi wa rangi, na wataona...

Kama wao watakuona kuwa mtu wa pekee; na kama wewe utawasimulia jinsi tulivyofanya sisi focolarine wa mwanzo, yale yanayotokea kwako, au ulijua kutoka kwa watu hawa hapa, kwa mfano, kwamba baada ya kutoa kitu ulipokea, na wewe unasimulia kuwa Yesu alisema ukweli, na wanakusikiliza, kwa sababu ni kitu kipya, ni jambo la kushangaza; ni dini inayoonekana kuwa mpya. Kwa sababu mara nyingi wanaamini kuwa dini ni kuabudu kidogo, kusali kidogo, lakini hawaoni uhai.

Kama wewe utawafanya waelewe kwamba umejawa na furaha kwa kuwa unaishi umoja, kwa sababu furaha hutokana na umoja, wao watashawishika kwa sababu unasimulia kwa matendo, unapaswa kufanya matendo. Hivi ndivyo unavyopaswa kuenenda.

## Tutajaribu!

Je, inawezekana kuwafanya vijana wengine wagundue tena kwenda kinyume cha mkondo? Pamoja, tafuteni mawazo kadhaa na mambo ya kuyatekeleza. Kwa mfano, tunawaandikia tukio lililotukia miaka kadhaa iliyopita:

« ***Julia Bluhm*** *ni msichana wa miala 14 anayeishi Maine (United States) na yuko kidato cha tatu. Siku moja Julia aligundua kuwa picha zilizokuwa kwenye baadhi ya magazeti zilikuwa zinawaaibisha rafiki zake wengi shuleni: matumizi ya "Photoshop" yanaficha mapungufu, inawafanya wote waonekana wakamilifu. Hasa msichana mmoja halipendi gazeti la 'Seventeen', gazeti la zamani na maarufu sana la 'teenager'. Alijisikia kusalitiwa akatuma ombi kwenye blog. Aliomba kwamba gazeti lijitahidi kuweka picha ya msichana wa kawaida, lisiweke mapambo.*

***Wasichana wengi walisisitiza huo wito.*** *Kwa ufupi, alisema: «sisi tunataka kuonekana jinsi tulivyo. Vielelezo vyenu ni vya hatari, kwa sababu siku zote kuna aliye mdhaifu anayetaka kujifananisha. Na hii inaweza kusababisha matatizo ya kula, mfadhaiko, kutojithamini».*

***Ni uchambuzi wa busara,*** *hivyo Julia, alishinda mapambano yake na mchapishaji wa Seventeen: hakuruhusu tena kamwe picha zenye mapambo.* »

## Tupo katika hatua gani?

*Ili* ***kulifikia lengo*** *ni lazima kufanya mazoezi kila siku na kutambua mabadiliko mazuri na magumu yaliyojitokeza. Itatusaidia hadi katika mkutano ujao, tutakapotenga muda wa kushirikishana mang'amuzi.*

Nilipata nafasi ya kutenda kadiri ya imani yangu hata kama kundi la umri wangu (marafiki, shuleni, kwenye michezo) walifikiri tofauti na mimi?

Ni magumu gani nilikutana nayo?

Kitu gani kilinisaidia?

Rafiki zangu walijibuje?

**Kwa ajili ya mlezi**

## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kutekeleza usafi wa moyo?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Ni kitu gani cha muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?